Viongozi watoa Risala za Idd ul Fitr Pwani

MWENYEKITI WA Kanu Wilayani Kwale Bw. Ali Masoud Mwakileo alipeleka Salamu zake za Idd el Fitr kwa Waisilamu wote na wananchi wote wa Kenya. Katika risala yake alisema "Waisilamu wamezidi kupata mafunzo zaidi katika mfungo wa wezi mtukufu wa Ramadhani na kwamba wana wajibu kuyatekeleza mafunzo hayo kwa nafsi zao, jamii zao, na taifa lao".

• Bw. Ali Mwasoud Mwakileo, mwenyekiti wa Kanu, Wilaya ya Kwale.

Katibu Mtendaji wa baraza kuu la Waisilamu Sheikh Mohammed Amana katika risala yake alisema "Mafunzo ya dini ya Kiisilamu pamoja na mafunzo ya mfungo wa Ramadhani ni msingi wa kutatua kila linalokabili taifa na watu wa Kenya".

Alisema mafunzo ya Ramadhani ni wajibu kutekelezwa kikamilifu ili dini ya Mwenyezimungu iweze kusonga mbele. Alitoa salamu zake za kheri kwa Mtukufu Rais Moi, serikali yake na chama kinachotawala cha Kanu.

Aliyekuwa mwenyekiti wa Chama cha Waisilamu Mombasa Bw. Hassanali Mussa Jetha katika risala yake ya Idd alisema "mwaka huu nina furaha zaidi kuona hasa lile jambo tulilokuwa tukilipigania la Kiwanja cha Makadara cha Maonyesho ya Sikukuu kimerejea pale tulipotaka, na hasa kwa furaha na kuwafurahisha watoto wetu ambao ndio viongozi wa siku zijazo". Bwana Jetha alipeleka salamu zake za udhati kwa Mtukufu Rais Moi, serikali na chama kinachotawala cha Kanu, pamoja na wananchi wote wa Kenya na kuwatakia kila heri.

• Bw. Hassanali Mussa Jetha, aliyekuwa mwenyekiti wa Muslim Association Mombasa.

Mwenyekiti wa baraza la chama cha National Union of Kenya Muslims (Nukem) Pwani Sheikh Ali Amin katika risala yake ya Idd alisema "Waisilamu wana shukurani kuu kwa serikali kwa vile wanavyopatiwa nafasi kamili ya kuabudu, na kuwekwa Kadhi Mkuu na makadhi kwa lengo la kusimamia sheria za Kiisilamu".

Alisema na kutoa mwito kwa Waisilamu kusonga mbele katika mafunzo na utumishi kwa taifa lao la Kenya, na umoja wa Kenya.

• Mwenyekiti wa Baraza la Nukem (Pwani) Sheikh Ali Amin

Katika risala yake ya baraza ya Idd mjini Mombasa Mwenyekiti wa baraza la Waisilamu Mombasa (Mombasa Muslim Association) Sheikh Ikram Ul Hassan alitoa mkono wa Idd kwa Mtukufu Rais Moi kwa niaba ya Waisilamu wote wa Mombasa, na wananchi wote wa Kenya.

Alisema "mwezi mtukufu wa Ramadhani umetakasa nyoyo za Waisilamu kwa kuitikia mafunzo ya Mwenyezimungu na kuwapa nafasi mpya ya kulitumikia taifa lao la Kenya chini ya maongozi ya busara ya Nyayo. Bw. ul Hassan alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Pwani Bwana Luka Galgalo na kusema "kwa muda mtupi Mkuu mpya wa Pwani ametekeleza mengi, na kwamba umoja wa Muslim Association upo pamoja naye katika kazi yake kubwa".

Bwana Ul Hassan alisema "tupo pamoja na serikali ya Kenya chini ya uwongozi wa Mpendwa, Mtukufu Rais Moi katika juhudi za kuondoa idhilali, mashaka na mateso ya viumbe, ugonjwa na matatizo yote ya taifa hili, na kwamba Waisilamu wa Mombasa tunamuhakikishia Mtukufu Rais Moi imani yetu kwake, kwa serikali yake na chama kinachotawala cha Kanu".

Alimpongeza Rais Moi na serikali yake kwa vile alivyokabili hali ya upungufu wa bidhaa humu nchini, na kumpa hekko kwa utumishi wake kwa wananchi wote wa Kenya.

OKWANYO AWAPONGEZA WAFANYI KAZI WA PIPELINE MOMBASA

WAZIRI wa Mafuta na Nguvu za Viwandani Bw. John Okwanyo ametilia mkazo umuhimu wa kampuni ya Kenya Pipeline na kuwataka wafanyi kazi wazidishe bidii katika kazi yao.

Alisema hayo baada ya ziara ya kutembelea afisi za kampuni hiyo hapa Mombasa akiandamana na Naibu wake Bw. Bakari Kassim Mwamzandi na Katibu wa Kuduma katika Wizara hiyo Bw. Mwiraria.

Anayeshikilia Madaraka ya Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo Bw. Otieno alimwambia Waziri kwamba kituo cha Mombasa cha Kenya Pipeline kinafanya kazi usiku mchana ili kusafirisha mafuta yote yanayosafishwa bila kuchelewa.

Mapema, Waziri alitembezwa katika kituo cha kusafishia mafuta cha Afrika Mashariki na Meneja wa Shughuli za kikazi wa kampuni hiyo Bw. Simion Obudo pamoja na Bw. David Kayanda Meneja wa Usimamizi wa Watumishi.

• WAZIRI JOHN OKWANYO

AKINA MAMA Kenya wanatwaa nafasi muhimu katika shughuli za Utalii. Hapa wafanyi kazi akina mama wa Hoteli ya Lawford, Malindi walijitokeza kwa mpiga picha wetu huko Malindi na kuwa timamu kuutumikia Utalii Kenya.

PICHA: NETA PEAL

BALOZI WA OMAN AMPONGEZA RAIS MOI

BALOZI wa Oman nchini Kenya Sheikh Abdulla Said Abdulla alipongeza maongozi mema na ya mfano mzuri yanayoongozwa na Mtukufu Rais Moi kwa raia wote wa Kenya.

Akihutubia sherehe moja wapo ya kuadhimisha sikukuu ya Idd el Fitr mjini Mombasa, Balozi huyo alisema maongozi ya Nyayo ya Mtukufu Rais Moi yamepata sifa katika mataifa yote ya Kiarabu, na ni jambo ambalo limevutia Waarabu wengi kuwa na imani kamili ya taifa hili na maongozi yake.

Alisema "Kenya na Oman ina uhusiano wa karne nyingi sana na kwamba ni lengo la Kiongozi wa Oman H. M. Sultan Qaboos bin Said Al Said kuzidi kuudumisha urafiki huu na ushirikiano kati ya Taifa la Oman na Kenya".

Alifahamisha na kusema "Oman ilijitokeza wazi wazi kushirikiana na wananchi wa Kenya katika kuumaliza ukoloni wa Kireno karne kadha mjini Mombasa na kwamba leo Oman ipo tayari na timamu kushirikiana na Kenya katika kuleta ushirikiana zaidi katika mambo ya faida kwa watu wa mataifa yetu mawili".

Alisema "Oman kama taifa changa linaloendelea limeweza kutekeleza mengi kwa maendeleo ya wananchi wake chini ya Maongozi ya busara ya Mtukufu H. M. Sultan Qaboos".

Alisema "maongozi ya Oman chini ya H. M. Qaboos bin Said Al Said ni mfano mkubwa kwa ulimwengu na kwamba juhudi za Rais Moi Kenya nazo pia ni mfano wa taifa changa linavyosonga mbele katika maendeleo, umoja, amani na upendo".

• BALOZI WA Oman nchini Kenya Sheikh Abdulla Said (wanne kutoka kushoto) akiwa pamoja na baadhi ya wazee wa Mombasa katika karamu. Wengine kutoka kushoto kwenda kulia ni Sheikh Mohammed Sultan Meskiry, Sheikh Mohammed Suleiman Mahruky, Sheikh Aboo Suleiman Mazrui. Kutoka kulia, wa kwanza Sheikh Mohammed Abeid, Sheikh Ali Masoud Riyami, na Sheikh Hamed bin Salim Rawahy.

HABARI KUTOKA LIBYA

NCHI ya Libya ni nchi yenye maendeleo ya kisasa na Utamaduni wa Ki-Islamu wenye msingi imara wa mafunzo ya Dini ya Uislamu. Nchi yenye kuvutia na ustawi mwema.

Haya yameelezwa na Bw. Jeffar Omar ambaye ni hivi majuzi tu tokea kufika huko Sirte, mmoja miongoni mwa miji ya Libya alikochukuliwa kwenda kufanya kazi za ufundi.

Alimwandikia mwakilishi wetu kumweleza kwamba wote wananchi wanaotoka Kenya wanafurahia maisha yao ya Libya na kuwaeleza kwamba wako katika hali ya furaha na ufanisi na wale ndugu zao waliowaacha Kenya wasitie wasiwasi wowote.

Bw. Jaffar Omar ni mzaliwa wa visiwa vya Bajuni na kabla ya kuondoka kwake kuende Libya alikuwa ni mmoja miongoni mwa fanya kazi katika ile kampuni inayojenga Daraja ya Nyayo.

Ni mvulana mashuhuri katika mtaa wa Inglani na mwenye marifiki wengi nchini Kenya kwa tabia yake njema ya uteshi hi.

Anawaomba marafiki zao wamwandikie barua wakipenda kujua hali ya maisha ya huku zaidi au kutaka kujiunga na yeye huko Libya. Anuwani yake ni Jaffar Omar, C.S.C. Cogifar-Camp, P.O. Box 59, Sirte, Libya.

Bw. Jaffar anawaahidi marafiki zake kwamba kila barua atakayoipata watawapitia majibu upesi iwezekenavyo.

Coastweek ** JEMBE

SWAHILI CROSSWORD NO.91



UNGA SAFI NO. 1

WA MAHINDI

KWENDA KULIA:
1. Majaribio
6. Mwisho
8. Bembeleza
9. Baba mdogo
10. Nyama iliyo ndani ya mfupa
12. .... havai moja
15. Kipindi cha usiku
17. Sehemu muhimu tumboni
18. Kumi mara kumi
20. Aina ya dawa za vidonge
21. Namna ya maradhi
22. Rai

KWENDA CHINI:
1. Aina ya mti
2. Wingi wa huyo
3. ..... ni deni
4. Kiungo cha ighali
7. Ufupi wa Salimu
11. Utomvu wa mmea wa mbungo
13. Panga gutu
14. Neno la kukataa
16. Joto, mwako
19. Umoja wa mataifa

JINA.......

SANDUKI LA POSTA.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 89:

[1] Mohamed Rashid, Sanduku la Posta 64, Malindi,

[2] Mustafa Rizik Faraj, Sanduku la Posta 98876, Mombasa,

[3] Swalah Karama Ali, Sanduku la Posta 80617, Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 89 —

KWENDA KULIA:
1. YAVUYAVU, 6. MAMANGU 7. NJE, 8. NYUFA, 10. AU, 11. BORA, 14. VOI, 15. MBIU, 16. BAKI, 17. LO.

KWENDA CHINI:
1. YAMINI, 2. VUMBUA, 3. YONGA, 4. VIUNGO, 5. NYEZA, 9. FUVA, 11. BIBO, 12. RIKA, 13. MBA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindo watatu wa kwanza kila mmoja atapatiwa 'T'-shirt moja ya Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LTD pamoja na ATTA LTD, Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Alhamisi tarehe 21.8.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.